



With support from




Federal Ministry
of Food
and Agriculture

by decision of the
German Bundestag


**Mwongozo wa Mafunzo kwa
Mameneja wa Mfumo wa Udhibiti wa
Ndani (ICS) kwa lengo la kupata
Cheti cha Kilimo Hai cha Umoja wa
Ulaya (EU).**



Viashiria Muhimu vya uthibitishwaji wa kikundi



Viashiria muhimu vya uthibitisho wa vikundi



The key indicators for group certification



Vijitabu



Cheti



Mkataba



(other)
CB aspects



Maelezo



Muongozo
wa ICS



Kumbukumbu




Usajili

	Vijitabu	Cheti	Mkataba	(other) CB aspects	Maelezo	Muongozo wa ICS	Kumbukumbu	Usajili
Wakulima	X	X	X	X	X	X	X	
Wajiri	X		X		X	X	X	
ICS-i	X		X		X	X	X	
ICS-m	X		X	X	X	X	X	
Washiriki	X		X	X	X	X	X	
Kikundi		X		X	X	X	X	X
CB		X	X	X				X
CB / AB / Comm		X						X


Yaliyomo Siku ya 3: Chombo cha uidhinishaji.

1. Je, chombo cha uidhinishaji kitaangalia nini?
2. Je, utaratibu wa uthibitishaji utafanyikaje?
3. Ni nini kinatokea iwapo wakaguzi watabaini matatizo?
4. Ni taarifa gani zinapatikana kwenye cheti?
5. Chombo cha utoaji vyeti nacho hukaguliwa?

Uthibiti wa nje na Uthibitishaji wa nje.




Udhibiti wa nje



- Weka wakaguzi wa ICS waliobobea
- Panga mipango kwa kuzingatia tathmini ya hatari
- Kila mwaka: hakiki maombi ya uzalishaji na mahitaji ya uwekaji lebo
- ✓ Utendaji kazi wa ICS
- Rikodi za ICS (ikiwemo ubadilishanaji wa taarifa)
- Kurudia ukaguzi
- Kushuhudia ukaguzi
- ✓ Uzalishaji wa kilimohai na wakulima
- Hatua za kuzuia
- Hatua za tahadhari
- ❖ Kutenganisha bidhaa na vitengo vya uzalishaji
- ❖ Kuchukua sampuli
- ✓ Maandalizi ya bidhaa za kilimo hai baada ya mavuno
- Utambuzi wa bidhaa za kilimohai
- Kutenganisha uzalishaji wa kilimo hai na usio wa kilimo hai

Uwezo wa kufuatilia


Udhibiti wa nje... lakini kabla ya kutoa taarifa.



CB


- Ni lazima kundi liwe limetoa yafuatayo:
 - ✓ Maelezo ya vitengo vya uzalishaji
 - ✓ Hatua zinazochukulia kuzingatia sheria na kanuni
 - ✓ Hatua za tahadhari
 - ✓ Uthibitisho kutoka kwa wanachama
 - ✓ Mkataba/makubaliano yaliyotiwa saini

Udhibiti wa nje: Njia na mbinu.



- ✓ Vitengo vya uzalishaji
- ✓ Majengo/Eneo la kazi
- Kaguzi
- ✓ Vitengo vya uzalishaji, vifaa, njia za usafirishaji, majengo
- ✓ Wanyama, mimea, bidhaa, viambato...
- ✓ Uwezo wa kufuatilia asili ya bidhaa, uwekaji lebo, vifaa vya ufungashaji
- Ukaguzi wa nyaraka ba kumbukumbu
- ✓ Uzalishaji
- ✓ Kuhusiana na ICS
- Mahojiano
- ✓ Uchukuaji wa sampuli na uchambuzi wa maabara
- ✓ Ukaguzi wa uwiano wa masi na uwezo wa kufuatilia asili ya bidhaa


Udhibiti wa nje... mwishoni: ripoti ya ukaguzi ...



- Itakuwa na angalau taarifa zifuatazo:
 - ✓ Rejea ya Kanuni ya EU 2018/848
 - ✓ Njia na mbinu zilizotumika
 - Angalia mbele
 - ✓ Matokeo
 - ✓ Hatua za kuchukuliwa na Kundi
 - ✓ Muda wa mwisho wa kutekeleza hatua hizo
 - ✓ Saini ya mkaguzi, meneja wa ICS, na mkulima pale inapohitajika

Ripoti za ukaguzi zinaweza kutolewa katika muundo wa kielektroniki au karatasi.

Udhibiti wa Nje: Mbinu na taratibu: uchukuaji sampuli



itatumia yafuatayo


- **Kuchukua sampuli na uchambuzi wa maabara**
- **Aidha, uchukuaji wa sampuli ni wa lazima iwapo kuna shaka ya matumizi ya dawa au mbinu zilizopigwa marufuku**
- **Maabara lazima ziwe zimeidhinishwa rasmi**
- ✓ Sampuli zisizopungua 2% ya idadi ya wanachama
- ✓ Aidha, uchukuaji wa sampuli ni wa lazima iwapo kuna shaka ya matumizi ya dawa au mbinu zilizopigwa marufuku
- 17025
- Na chombo cha utoaji ithibati kilichoidhinishwa
- ✓ Kuhusu uchunguzi wa viuatilifu, mbinu zinazotumika zitahusisha angalau viambato amilifu vinavyofuatiliwa rasmi na Nchi Wanachama wa EU
- ✓ Uchukuzi wa sampuli unaweza kukabidhiwa kwa wachukuzi wa sampuli waliothibitishwa.

Mamlaka ya udhibiti au chombo cha uthibitisho kitachukua na kuchambua sampuli ili kubaini matumizi ya bidhaa na vitu visivyoidhinishwa kwa uzalishaji wa kilimo hai, kukagua mbinu za uzalishaji ambazo hazizingatia kanuni za uzalishaji wa kilimo hai, na kugundua uwezekano wa uchafuzi unaosababishwa na bidhaa na vitu visivyoidhinishwa kwa uzalishaji wa kikaboni.

Mamlaka au chombo cha udhibiti kitachukua na kuchunguza sampuli ili kubaini matumizi ya bidhaa na vitu visivyoruhusiwa katika uzalishaji wa kilimohai, kukagua mbinu za uzalishaji zisizoendana na kanuni za uzalishaji wa kilimohai, au kubaini uwezekano wa uchafuzi unaotokana na bidhaa na vitu visivyoruhusiwa kwa ajili ya uzalishaji wa kilimohai.

✓ .


Udhibiti wa nje... kabla ya kuthibitisha....



Shirika la Ukaguzi (CB) lazima lihakikishe kuwa:

- **Kundi linazingatia kanuni za uzalishaji**
- **Bidhaa za kundi zimewekewa lebo kwa mujibu wa kanuni za uwekaji lebo**
- **Wakandarasi wadogo wanajumuishwa katika mfumo wa udhibiti**
 - ✓ **Pamoja na au bila uthibitisho binafsi**
- **Vikundi vinavyobadilisha CB**
- ✓ **Vyeti vilivyotolewa awali ni halali**
- ✓ **Masuala ya kutotimiza masharti yaliyobainishwa awali (miaka 3 iliyopita) yameshughulikiwa**
- ✓ **Misamaha maalum imetolewa au inashughulikiwa**
- **Iwapo cheti cha kikundi kimeondolewa katika kipindi cha miaka miwili iliyopita**

Udhibiti wa nje... na kisha kuthibitisha...




Cheti kina taarifa zifuatazo:

- ✓ Shughuli
- ✓ Makundi ya bidhaa
- ✓ Bidhaa
- ✓ Kilimo hai
- ✓ “katika mabadiliko /kipindi cha mpito”
- ✓ Muda wa kutumika
- ✓ Orodha ya wanachama
- ✓ Jina
- ✓ anuani
- ✓ Kiasi (kg, lita au hekari)
- ✓ Orodha ya majengo au viteng
- ✓ Taarifa kuhusu utoaji wa kazi kwa wakandarasi wadogo
- ✓ Taarifa nyingine

Lazima

Exercise: via internet: download the certificate of the operator Interfood 60, in Serbia, certified by Ecocert
Via (not yet available on TRACES)


Udhibiti wa nje... na kisha kusasisha tovuti



✓ Tovuti

- Orodha ya vikundi vilivyothibitishwa
- ✓ Jina na anwani ya kikundi pamoja na idadi ya wanachama wake
- ✓ Namba ya Cheti
- ✓ Kundi la bidhaa
- ✓ Hali ya uthibitisho Certification status
- ✓ Muda wa kutumika
- Orodha itasasishwa mara moja kila baada ya mabadiliko yoyote
- Iwapo kutakuwa na uondoaji, taarifa kuhusu cheti zitahifadhiwa kwenye orodha kwa muda wa miaka 5 baada ya uondoaji
- Viwango vya uzalishaji na hatua za udhibiti

Udhibiti wa nje... na kisha kuboresha mfumo wa tehamu (Kanzi data)



- ✓ **Kanzi data itajumuisha angalau taarifa zifuatazo (chaguzi husika):**
 - ✓ Ukubwa wa kikundi
 - ✓ Jina na anwani ya kila mwanachama
 - ✓ Hali ya ubadilisho
 - ✓ Kiwango cha hatari
 - ✓ Jina na anwani za wakandarasi wadogo
 - ✓ Majira ya nukta ya eneo la uzalishaji, na majengo yote
 - ✓ Ruhusa zilizotolewa
 - ✓ Ripoti za ukaguzi
 - ✓ Ripoti za maabara
 - ✓ Barua ya kutokufikia kanuni/viwango
 - ✓ Ankara

Kipindi cha mabadiliko na utambuzi na kipindi kilichopita

Utambuzi wa kipindi kilichopita.

(Nje ya EU)

CB zinaweza kutoa "utambuzi wa kipindi cha awali kama sehemu ya kipindi cha ubadilishaji", lakini chini ya masharti magumu.

- Nyaraka za kina kutoka kwa mwendeshaaji kuthibitisha kuwa ardhi hiyo ilikuwa ya asili/haijafanyiwa matibabu yoyote kwa miaka 3 iliyopita: ramani, taarifa za eneo (geolocation), picha, na maelezo ya uzalishaji wa sasa.
- Shirika la Uthibitishaji (CB) litafanya uchambuzi wa hatari na uchambuzi wa sampuli kulingana na hatari, na kutoa ripoti ya ukaguzi baada ya kufanya ukaguzi wa eneo ili kuthibitisha usahihi na uwiano wa taarifa




Usimamizi wa ubadilisho kwa Kundi la Opareta (GoO) ICS

Taratibu za ICS za kusajili na kuidhinisha wanachama wapya au kuongeza sehemu/shughuli kwa wanachama waliopo na kushughulikia ubadilisho

ICS huchunguza na kukusanya nyaraka kwa wanachama/viwanja vyote vipya vilivyopendekezwa kwa ajili ya utambuzi wa nyuma.

Utambuzi wa mabadiliko ya hadhi kuanzia tarehe ya nyuma unaweza kuidhinishwa na CB pekee baada ya kufanyika kwa uhakiki wa eneo husika unaozingatia tathmini ya hatari.

Udhibiti wa nje... vipi ikiwa ripoti ya maabara itaonyesha kuwepo kwa vitu vilivyopigwa marufuku?



Chunguza

- Kutambua
 - ✓ Chanzo
 - ✓ Sababu
 - Kuthibitisha kama opereta
 - ✓ Alitumia bidhaa zilizoidhinishwa pekee
 - ✓ Kuhusu kuepuka uchafuzi na ubadilishaji
 - Imetambua hatari
 - Alichukua hatua zake mwenyewe

Mjulishe mwendeshaji kuwa bidhaa siyo za kilimohai wakati

- Mwendeshaji ametumia bidhaa nyingine
- Hakuchukua hatua zake mwenyewe
- Amepuuza masuala ya awali

Udhibiti wa nje... vipi iwapo Shirika la Uthibitishaji (CB) litabaini kutozingatia masharti?

Taarifa zilizothibitishwa
kuhusu kutokufikiwa
kwa kanuni
kumakoathiri uadilifu
wa bidhaa za kilimo
Hai

CB




GoO



Shirika la Uthibitishaji (CB) litahakikisha kuwa

- Rejeleo la uzalishaji wa kilimohai litaondolewa kwenye bidhaa husika
- Chanzo na kiwango cha ukiukwaji vinabainishwa
 - ✓ Mafungu mengine
 - ✓ Mashamba mengine
- Anzisha majukumu ya GoO
- GoO inachukua hatua za
 - ✓ Rekebisha hali isiyokidhi matakwa
 - ✓ Huzuia matukio kama hayo kujirudia
- Iwapo kutakuwa na ukiukwaji mkubwa, au wa kujirudia-rudia au kuendelea
 - ✓ Cheti cha GoO's
 - Kitasimamishwa or
 - Kitaondolewa

Mapungufu ya Mfumo wa Udhibiti wa Ndani / Athari za Kushindwa kwa Mfumo wa Udhibiti wa Ndani.




Mamlaka za udhibiti zitabatilisha cheti cha kundi zima iwapo kasoro katika uanzishwaji au uendeshaji wa Mfumo wa Udhibiti wa Ndani (ICS) zitaathiri uhalisi wa bidhaa za kilimo hai na zile zilizo katika kipindi cha mpito kuelekea kilimo hai—hasa pale ambapo kuna kushindwa kugundua au kushughulikia ukiukwaji wa kanuni unaofanywa na wanachama binafsi wa kundi hilo.

Mapungufu ya ICS ni, kwa mfano

Kutofanya ukaguzi wa ndani kwa asilimia 100 kila mwaka
Tofauti kubwa kati ya matokeo ya ukaguzi wa ndani na ule wa nje
Mapungufu makubwa katika kuchukua hatua stahiki pale kunapokuwa na hali ya kutokidhi vigezo (NC)
Kuchakata au kuuza bidhaa kutoka kwa wanachama waliosimamishwa au walioondolewa
Kuongeza wanachama au vitengo vipya kwenye orodha bila kufuata taratibu
Idadi isiyotosheleza ya wakaguzi wa ndani wenye uwezo stahiki.

Tathmini ya haraka

Viashiria muhimu vya uthibitisho wa vikundi



Viashiria muhimu vya uthibitisho wa vikundi



Vijitabu



Cheti



Mkataba



(nyenginezo)
CBs



Maelekezo



Muongozo wa
ICS



Kumbukumbu



Usajili

Wakulima	X	X	X	X	X	X	X	
Waajiri	X		X		X	X	X	
ICS-i	X		X		X	X	X	
ICS-m	X		X	X	X	X	X	
Wadau	X		X	X	X	X	X	
Kikundi				X	X	X	X	X
Wahibitishaji (CB)		X	X	X				X
CB/AB/Comm		X						X

Uwiano wa kiasi.

Rekodi zinazohitajika ili kufanya ukaguzi wa uwiano wa kiasi

Ukaguzi wa uwiano wa kiasi utahusu vipengele vifuatavyo, vikithibitishwa na nyaraka zinazofaa, ikiwa ni pamoja na rekodi za akiba na za kifedha pale inapohitajika:

I. Aina na kiasi cha bidhaa zilizowasilishwa kwenye kitengo na, inapohitajika vifaa vilivyonunuliwa na matumizi ya vifaa hivyo, pamoja na hali ya bidhaa husika;

II. Aina na kiasi cha bidhaa zilizohifadhiwa katika eneo husika, ikiwa ni pamoja na wakati wa kufanya ukaguzi halisi wa papo hapo;

III. Aina na kiasi cha bidhaa zilizotoka kwenye kitengo cha waendeshaji au makundi ya waendeshaji kwenda kwenye eneo la mpokeaji au vituo vya kuhifadha;

IV. Kwa waendeshaji au makundi ya waendeshaji wanaonunua au kuuza bidhaa bila kuzihifadhi au kuzifanyia maandalizi, aina na kiasi cha bidhaa zilizonunuliwa na kuuzwa;

V. Kiasi cha mavuno ya bidhaa zilizopatikana, kukusanywa au kuvunwa katika mwaka uliopita;

VI. Makadirio au kiasi halisi cha mavuno ya bidhaa zilizopatikana, kukusanywa au kuvunwa katika mwaka huu;

Idadi na/au uzito wa mifugo iliyofugwa katika mwaka huu na mwaka uliopita;

Hasara yoyote, ongezeko au upungufu wa kiasi cha bidhaa katika hatua yoyote ya uzalishaji, uandaaji na usambazaji;

Jumla ya uzalishaji wa shamba kwa upande wa bidhaa za kilimohai na zisizo za kilimohai

Meneja wa ICS hupata haya wapi?

- (a)
- (b)
- (c)
- (d)
- (e)
- (f)
- (g)
- (h)
- (i)

Ukaguzi wa ufatiliaji wa asili ya bidhaa.

Kumbukumbu zinazohitajika ili kufanya ukaguzi wa ufuatiliaji

Mbali na vipengele vingine vinavyoweza kuhitajika na mamlaka au chombo cha udhibiti, ukaguzi wa ufuatiliaji unapaswa kujumuisha vipengele vifuatavyo, vinavyothibitishwa na nyaraka husika ikiwemo kumbukumbu za hisa na za kifedha:

- (a) Jina na anwani ya msambazaji na, pale inapohitajika, ya mmiliki au muuzaji, au mtoaji nje wa bidhaa.
- (b) Jina na anwani ya mnunuzi na, pale inapohitajika, ya mnunuzi au muingizaji wa bidhaa.
- (c) Cheti cha msambazaji kwa mujibu wa sheria ya utekelezaji iliyopitishwa chini ya Kifungu cha 45(4) cha Kanuni (EU) 2018/848.
- (d) Taarifa zilizotajwa katika aya ya kwanza ya kipengele cha 2.1 cha Kiambatisho III cha Kanuni (EU) 2018/848.
- (e) Utambulisho sahihi wa kundi (lot identification).
- (f) Kwa wasindikaji, taarifa muhimu zinazoweza ufuatiliaji wa ndani na kuhakikisha hadhi ya kilimo hai ya viambato

Meneja wa ICS hupata haya wapi?

- (a)
- (b)
- (c)
- (d)
- (e)
- (f)

Kumbukumbu za hisa na za kifedha zinazopaswa kuhifadhiwa na GG

Kumbukumbu zinazopaswa kuhifadhiwa na GoO

1. Opareta na GoO wanapaswa kuhifadhi nyaraka zote muhimu, ikiwemo kumbukumbu za hisa na za kifedha, ambazo zitawawezesha mamlaka husika au, pale inapohitajika, mamlaka au vyombo vya udhibiti kufanya hasa ukaguzi ufuatao:

- (a) Ukaguzi wa hatua za kinga na tahadhari zilizochukuliwa kwa mujibu wa Kifungu cha 9(6) na Kifungu cha 28 cha Kanuni (EU) 2018/848.
- (b) Ukaguzi wa ufuatiliaji kwa mujibu wa Kifungu cha 1(4) cha Kanuni ya Utekelezaji (EU) 2021/771.
- (c) Ukaguzi wa uwiano wa uzalishaji (mass balance check) kwa mujibu wa Kifungu cha 1(5) cha Kanuni ya Utekelezaji (EU) 2021/771.

2. Nyaraka zinazopaswa kuhifadhiwa kwa madhumuni ya ukaguzi uliotajwa katika aya ya 1, kipengele (a), zinapaswa kujumuisha hasa nyaraka zinazothibitisha kwamba opareta au GoO kuchukua hatua zinazolingana na stahiki ili:

- (a) Kuzuia wadudu na magonjwa;
- (b) Kuepuka uchafuzi kwa bidhaa na vitu ambavyo havijaruhusiwa kutumika katika uzalishaji wa kikaboni kwa mujibu wa Kanuni (EU) 2018/848 na kuchanganyika na bidhaa zisizo za kikaboni.

Meneja wa ICS hupata haya wapi?

1.

- Uzalishaji na maandalizi:
- Kumbukumbu za hisa:
- Kumbukumbu za kifedha:

2.

- Ngazi ya wakulima
- Katika ghala
- Katika maeneo ambako shughuli za maandalizi zinafanyika”?



With support from



Federal Ministry
of Food
and Agriculture

by decision of the
German Bundestag

ASANTE!

IFOAM
ORGANICS
INTERNATIONAL



With support from



Federal Ministry
of Food
and Agriculture

by decision of the
German Bundestag

Maswali & Majibu

IFOAM
ORGANICS
INTERNATIONAL